


ASb
approved




Kiswahili


Hadithi Za Bibi

Ursula Nafula


Marleen Visser



Sote tulikuwa
tumekusanyika nyumbani
kwa bibi kuzisikiliza
hadithi zake. Tuliketi
karibu na meko.
Bibi alianza kutusimulia,
"Sungura na Tembo
walikuwa majirani pia
marafiki.




Sungura alipenda uyoga,
lakini alikuwa mvivu sana.
Alizoea kuiba uyoga wa
Tembo. Tembo alikuwa
amepanda ndizi na
malenge mwaka huo. Kwa
hivyo, Sungura hakupata
uyoga.



Sungura alikosa chakula
kwa siku nyingi. Aliamua
kuiba ndizi za Tembo.
Tembo aligundua kwamba
ndizi zake zilikuwa
zikiibwa. Alimwendea
Sungura na kusema,
"Kuna mtu fulani
ananiibia."



Sungura aliuliza, "Ni nani mwizi?" Tembo alianza kuimba, "Nitamshika mwizi! Aaa! Nitamshika mwizi! Ooo!" Sungura alikuwa na wasiwasi sana.



Tembo alimwuliza Kima kumchungia shamba lake. Lakini, Sungura hakuiba mchana wala usiku huo. Hakuiba siku iliyofuata wala usiku uliofuata. Kima alichoka kuchunga.



Siku iliyofuata, Sungura
alienda tena katika
shamba la Tembo kuiba.
Tembo alipoenda kukagua
mimea yake, Sungura
alijificha katika matawi ya
malenge.




Tembo alipoyaona matawi yakitingika, alianza kuimba, "Nimemshika mwizi! Aaa! Nimemshika mwizi! Ooo!" Tembo alitafuta kila sehemu lakini hakumpata mwizi.



Siku moja, Sungura
alipokuwa akila mazao ya
Tembo shambani, Tembo
aliwasili. Sungura aliruka
na kujificha ndani ya
malenge moja kubwa.




Tembo aliiона ile malenge
kubwa akasema, "Ooo!
Hapa kuna malenge
kubwa. Itakuwa chakula
changu cha mchana."
Aliimeza mara moja!



Sungura alijaribu kuruka nje ya malenge, lakini hakuweza. Tembo alipohisi kitu kikiruka tumboni mwake, alijiuliza, "Hii ni malenge ya aina gani inayoruka tumboni mwangu?"



Tembo aliitema nje ile malenge. Kabla kuikagua, Sungura alijitosa nje ya malenge na kutoroka. Tembo hakuwahi kumshika mwizi."



Bibi alisema, "Na huo ndio
mwisho wa hadithi."
"Asante bibi," tulimjibu
pamoja. Tuliviweka
vikombe vyetu vya
maziwa, kisha tulienda
kulala tukiwaza juu ya
hadithi za bibi.

You are free to download, copy, translate or adapt this story and use the illustrations as long as you attribute in the following way:

Hadithi Za Bibi

Author - Mutai Chepkoech

Translation - Ursula Nafula

Illustration - Marleen Visser

Language - Kiswahili

Level - First paragraphs

© African Storybook Initiative 2016

Creative Commons: Attribution 4.0

Source www.africanstorybook.org

